

## **Mradi Namba 6567: HABARI KWA UMMA**

Kiasi cha **Sh. 940,000,000** kiliombwa kwa ajili ya kukusanya, kuchakata, kuandaa na kusambaza habari na taarifa kwa wananchi kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa Serikali ikiwemo Sera, Mikakati, Miradi na Programu zinazotekelezwa na Serikali. Katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mradi huu ni:

- (i) Kukusanya, kuchakata, kuandaa na kusambaza habari na taarifa kwa wananchi kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali ikiwemo Sera, Mikakati, Miradi na Programu zinazotekelezwa na Serikali; na
- (ii) Kukusanya taarifa za mrejesho kutoka kwa wananchi kwa lengo la kupata maoni ya wananchi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Hadi kufikia **tarehe 31 Disemba, 2022** Wizara ilipokea jumla ya **Sh 420,797,259.99/-** sawa na asilimia **44.8** ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Mradi tajwa. Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi husika ni kama ifuatavyo: -

(i) Ununuzi wa Magari matatu – aina ya Toyota Landcruiser Prado TXL Manual na Toyota Hilux Double Cabin Pick Up mbili (2) ambapo Sh. **347,628,409.99** zimetumika. Pia kiasi cha Sh. **73,168,850.00/-** kwa ajili ya kulipia kifaa cha kurushia matangazo mubashara aina ya Live U.

(ii) Vipindi ishirini (20) vya Televisheni vinavyohusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo viliandaliwa na kurushwa TBC1. Vipindi hivi vilihusu Kilimo na Umwagiliaji, Viwanda, Ujenzi, Madini na Upanuzi wa Bandari ya Tanga.

(iii) Kuratibu Mikutano ya Taasisi za Serikali kutoa taarifa za utekelezaji kupitia vyombo vya habari. Jumla ya Taasisi 37 ziliratibiwa na kutoa taarifa kwa umma kuhusu utekelezaji wa shughuli zake.